**RANGI NYEKUND**

## Ushirika wa vitu

GEN 3

**RANGI NYEKUND**

## Utamaduni wa kutoa

GEN 3 | CHIPKIZI WA UMOJA

KUTOKA KWENYE KANUNI YA GEN 3

***"Mungu alitupatia mali za dunia ili tuzitumie kwa manufaa ya wote.*** *Kama mimea ichukuavyo chakula kinachohitajika kutoka ardhini, gen 3 wasichana na wavulana wanataka kumiliki vile vilivyo muhimu tu.* ***Wanajitahidi kufanya ushirika wa vitu, wa kiroho na wa vipaji.*** *Wanataka kusiwe na kitu kinachochukua nafasi ya Mungu moyoni mwao".*

KUTOKA KWENYE KANUNI YA GEN 3

*"Ili kufikia malengo yao, gen 3 pamoja na Chipkizi wa Umoja, wanafuata njia mbali mbali wanazoziita 'njia ndogo', na wanahamasisha* ***shughuli*** *na ubunifu mbali mbali,* ***katika ngazi ya mahali na katika ngazi ya kidunia.***

USHIRIKA WA MALI ZA KIROHO

### *Ushirika wa mang'amuzi*

*"Ni muhimu sana kuishi Neno la Uzima. Lakini haitoshi.* ***Sisi tunaitwa kuweka katika ushirika mang'amuzi yetu".***

NJIA NDOGO YA RANGI NYEKUNDU

### *Njia za umoja wa dunia*

*"Tuishi na tueneze utamaduni wa kutoa kama* ***kiuasumu cha ulaji.*** *Tutengeneze* ***mtandao wa upendo unaounganisha chipkizi wa nchi mbali mbali duniani*** *kwa kupitia ushirika wa vitu.* *Tukusanye pesa ili kutegemeza elimu ya chipkinzi(vijana) na kwa ajili ya mahitaji mengine".*

USHIRIKA WA MALI

### *Ushirika wa vitu duniani kote*

*"Ukurasa wa waktisto wa kwanza unatuvutia sana, wakati* ***walikuwa moyo mmoja na roho moja*** *kule Yerusalemu.* *Na hakuna aliyesema nilivyonavyo ni mali yangu,* ***waliweka kila kitu katika ushirika na hakuna aliyepungukiwa kati yao".***

MIRADI TEENS4TEENS

### *Miradi midogo ya mshikamano*

*"Tunategemeza miradi midogo ya mshikamano inayoitwa "****Teens4Teens****",* ***ambayo kwayo*** *tunategemeza wavulana na wasichana ambao kwa sababu ya ugumu wa kiuchumi na kijamii, hawana uwezekanao wa kwenda shule".*

KUPATA MARA MIA KWA INJILI

***"Kutoa kwetu kutafungua mikono ya Mungu naYe atatujaza kwa wingi.***

*Anayetoa, aliyeishi katika upendo, ana zawadi ya uhai hapa duniani. Kwa namna hii tunaweza kuwasaidia watu wengi wanaohitaji msaada".*

DHARURA ZA KIDUNIA

### *Mtazamo uliowazi kwa dunia*

*"Kitu kingine tunachofanya ni kuangalia vizuri, kila siku, yanapotokea majanga kama kwa mfano, kuzuka kwa moto, tetemeko la ardhi, mafuriko au maafa mengine kama vita.* *Tunakusanya pesa kwa njia zote ili kuwasaidia wavulana na wasichana wanaojikuta katika majanga kama hayo, ili wasiharibikiwe au kupata uchungu zaidi".*